# Kufahamu Matokeo ya Kipimo Chako cha Homa ya Manjano B*

**Jopo la vipimo vya damu la Homa ya Manjano B linajumuisha vipimo vitatu. Matokeo yote matatu lazima yajulikane ili kuthibitisha hali yako. Ifuatayo ni jedwali lililo na ufafanuzi wa kawaida zaidi wa matokeo ya kipimo, lakini matokeo ya kipimo yasiyo ya kawaida yanaweza kutokea.**

TAFADHALI KUMBUKA: jedwali hili halilengi kutoa ushauri wa matibabu. Ongea na mhudumu wako wa afya kwa ajili ya ufafanuzi kamili na kupata nakala iliyochapishwa ya matokeo ya kipimo chako.

| **HBsAg** Sehemu ya Homa ya Manjano B Kipimo cha Antijeni | **Dawa za kukinga Homa ya Manjano B** (HBsAb) Sehemu ya Homa ya Manjano B Kipimo cha Kingamwili | **Dawa za kukinga Homa ya Manjano B** (HBcAb) Msingi wa Homa ya Manjano B Kipimo cha Kingamwili | **Maana ya matokeo** | **UNACHOHITAJI KUFANYA** |
|---|---|---|---|---|
| − | − | − | **Huna kingamwili/hujalindwa**<br>• Huna maambukizo na hujaambukizwa katika siku zilizopita.<br>• Upo katika hatari ya maambukizo ya homa ya manjano B. | **Chanjo inahitajika** |
| − | + | − | **Una kingamwili/umelindwa**<br>• Hujaambukizwa.<br>• Una kingamwili kwa sababu ya chanjo ya homa ya manjano B. | **Hakuna chanjo inayohitajika** |
| − | + | + | **Una kingamwili kwa sababu ya maambukizo asili**<br>• Umepata nafuu kutoka kwa maambukizo ya awali ya homa ya manjano B.<br>• Huwezi kuwaambukiza wengine. | **Hakuna chanjo inayohitajika**<br>• Waambie madaktari wako wote kuhusu matokeo ya kipimo chako cha homa ya manjano B.<br>• Ongea na daktari wako kuhusu kutumia dawa za kuboresha kingamwili kwa sababu zinaweza kuongeza hatari ya kutokea tena kwa homa ya Manjano B. |
| + | − | + | **Umeambukizwa**<br>• Una virusi vya homa ya manjano B katika damu yako.<br>• Unaweza kusambaza virusi vya homa ya manjano B kwa wengine. | **Unahitaji kipimo zaidi**<br>• Tafuta daktari kwa ajili ya tathmini na kipimo zaidi.<br>• Waambie madaktari wako wote kuhusu matokeo ya kipimo chako cha homa ya manjano B.<br>• Hakikisha mchumba wako na wanaoishi na wewe wamepimwa na wamepokea chanjo. |
| − | − | + | **Unaweza kuambukizwa**<br>• Matokeo si wazi-maambukizo ya homa ya manjano ya sasa au yaliyopita. | **Unahitaji kipimo zaidi**<br>• Tafuta daktari kwa ajili ya tathmini na kipimo zaidi.<br>• Waambie madaktari wako wote kuhusu matokeo ya kipimo chako cha homa ya manjano B.<br>• Ongea na daktari wako kuhusu kutumia dawa za kuboresha kingamwili kwa sababu zinaweza kuongeza hatari ya kutokea tena kwa homa ya Manjano B.<br>• Hakikisha mchumba wako na wanaoishi na wewe wamepimwa na wamepokea chanjo. |

*Taarifa katika jedwali hili haitumiki kwa watu ambao huenda wana homa kali ya manjano B (au maambukizo ya hivi karibuni).

Hep B Hub
doh.wa.gov/hepbhub

Washington State Department of Health

DOH 420-434 October 2022 Swahili
Ili kuomba hati hii katika muundo mwinginee, piga simu kwa 1-800-525-0127.
Kwa watu walio na ulemavu au matatizo ya kusikia, tafadhali piga simu kwa 711 (Washington Relay) au tuma barua pepe civil.rights@doh.wa.gov.